

Magaidi wa MNR

P 4 wataangamizwa Mzalendo

Ndugu Mhariri,

13/9/87

Naomba niseme machache yanayohusu makaburu wa Afrika ya Kusini na magaidi wanaowatumia katika kutishia uhuru wa umma wa Waafrika. Wananchi wa Tanzania tumepokea kwa majonzi makubwa taarifa ya mauaji ya kinyama yaliyofanywa na magaidi wa M.N.R. nchini Msumbiji na kuua mamia ya wananchi wasio na hatia.

Nategemea wapenda amani pote duniani wanaungana nasi katika majonzi hayo na kulaani kitendo hicho cha kinyama na kuongeza misaada ya

hali na mali kwa wananchi wa Msumbiji.

Katika sikukuu moja ya krismas na mwaka mpya nimewahi kumsikia Botha akipayuka kwenye Radio kuwa anamwomba Mungu baba atujalie mapendo na amani.

Matunda ya makaburu dhidi ya wazalendo ndiyo mapendo na amani? Watanzania hatutasikiliza uwongo wowote atakaosema Botha hata tukimkuta kanisani. Nao magaidi wa Msumbiji waelewe hata wakifanya ukatili kiasi gani hawatatishia umoja wa wananchi wa Msumbiji kama hawaamini waulize Wareno ambao waliwachoma moto wazalendo wengi, lakini mwisho wao walishuhudia bendera ya wana Mapinduzi wa FRELIMO ikipandishwa.

S.L.P. 4,
PERAMIHO.

CHARLES LIBOMA